Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
# MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA NNE

**021** **KISWAHILI**

(Kwa watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 3** **Mwaka: 2025**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na moja (11)**.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na B na maswali **mawili (2)** kutoka sehemu C ambapo swali la **tisa (9)** ni la lazima.
3. Sehemu A ina alama **kumi na sita (16)**, sehemu B alama **hamsini na nne (54)** na sehemu C ina alama **thelathini (30)**.
4. Zingatia maelekezo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
5. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa **bluu** au **mweusi**.
6. Vifaa vya mawasiliano na vitu visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
7. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 16)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Katika vipengele (i) hadi (x), chagua herufi ya jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu hilo katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Ni taarifa zipi zinaweza kupatikana katika kamusi kati ya hizi?

A Neno, maana, matamshi na matumizi ya semi
B Maana, neno, mazungumzo na matumizi ya semi
C Matumizi ya semi, matamshi, maana na mazungumzo
D Matamshi, mazungumzo, maana na kidahizo
E Kidahizo, matamshi, mazungumzo na semi

(ii) "Juma anaendesha baiskeli yake polepole." Kiarifu cha sentensi hii kimejengwa na mfuatano upi wa vipashio?

A Kiima, chagizo na shamirisho
B Kitenzi kishirikishi, shamirisho na chagizo
C Kiarifu, kiima na chagizo
D Shamirisho, chagizo na kitenzi kikuu
E Kitenzi kikuu, shamirisho na chagizo

(iii) "Tutakuja kumpokea kwenye uwanja wa ndege." Kazi ya kielezi kinachojitokeza kwenye sentensi hii ni ipi kati ya hizi?

A Kueleza idadi
B Kueleza mahali
C Kueleza namna
D Kueleza wakati
E Kueleza nafsi

(iv) Tamathali ipi ya semi hufananisha mambo kwa kutumia viunganishi?

A Tashititi
B Sitiari
C Nidaa
D Tashibiha
E Tabaini

(v) Tamathali ipi ya semi inatawala katika wimbo ufuatao?

*Ze ndi ndi ndi*!
*Tolly ndi*!
*Ndi ndi ndi ndi*!
*Tolly ndi*! x4

A Tabaini
B Taniaba
C Tashibiha
D Takriri
E Tashihisi



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(vi) Neno lipi linadhihirisha kauli ya kutendeka katika kitenzi pika?

A Pikia
B Pikiwa
C Pikika
D Pikwa
E Pikisha

(vii) Yupi kati ya wafuatao anajishughulisha na kusoma, kuchambua na kutoa maoni katika kazi za sanaa?

A Mdhamini
B Mtunzi
C Mhariri
D Msomaji
E Mhakiki

(viii) Hatua mojawapo ya uendelezaji wa lugha ili itumike kitaifa na kimataifa ni kuisanifisha. Jambo lipi kubwa linalofanywa katika hatua hii kati ya yafuatayo?

A Kupunguza maneno ya kukopa
B Kuondoa tofauti za kimsamiati
C Kuifanya itumike na jamii ndogo
D Kuweka tofauti za matamshi
E Kuidhinisha tofauti za maneno

(ix) Ni kwa namna gani tungo hutofautiana na sentensi?

A Tungo zote ni sentensi lakini sentensi zote si tungo
B Sentensi haitoi taarifa kamili lakini tungo hutoa taarifa kamili
C Sentensi ni miongoni mwa tungo lakini si kila tungo ni sentensi
D Tungo sharti ikamilike lakini sentensi si lazima ikamilike
E Tungo ni ndefu sana lakini sentensi ni fupi sana

(x) Jambo lipi **si muhimu** katika uandishi wa kadi ya mwaliko?

A Jina la mwandishi na mwalikwa
B Idadi ya waalikwa
C Tarehe ya tukio
D Kusudi la tukio
E Mahali tukio linapofanyika


Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

2. Oanisha mifano ya tamathali za semi iliyo katika **Orodha A** na tamathali husika zilizo katika **Orodha B** kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kijitabu chako cha kujibia.

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|
| (i) Kilio cha mama mfiwa kilisikika mithili ya king'ora. | A Mjalizo |
| (ii) Haba na haba hujaza kibaba. | B Tashihisi |
| (iii) Misitu ni uhai. | C Tasfida |
| (iv) Shangazi amejifungua salama. | D Tabaini |
| (v) Upepo mkali ulipiga miluzi kila ulipogonga kingo za mito. | E Tashibiha |
| (vi) Binadamu hupanga, Mungu hupangua. | F Onamatopea |
| | G Sitiari |
| | H Takriri |

**SEHEMU B (Alama 54)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. (a) Tumia mzizi chez- kuunda vitenzi viwili kwa kila kauli kama zilivyoorodheshwa:
   (i) Kauli ya kutendeana
   (ii) Kauli ya kutendana
   (iii) Kauli ya kutendeka
   (iv) Kauli ya kutendewa

   (b) Unda nomino moja kwa kila kitenzi.
   (i) Zaa (ii) Kimbia (iii) Shikilia
   (iv) Elekeza (v) Penda

4. (a) Fafanua vyanzo vinne vya misimu kwa kutoa mfano mmoja kwa kila chanzo cha msimu husika.

   (b) Eleza maana mbili kwa kila neno.
   (i) Kaka (ii) Kito (iii) Mkaa
   (iv) Mkwaju (v) Babu

5. Bainisha viambishi vya o - rejeshi katika kila sentensi kwa kuvipigia mstari kisha taja ngeli husika kwa kila kirejeshi.
   (a) Udongo ulioleta umekauka
   (b) Kioo kilichovunjika kimeletwa
   (c) Karatasi zilizokauka zimetumika
   (d) Mlimokuwa mna joto sana
   (e) Kijana atakayeshinda atapewa zawadi

Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

(f) Gazeti lililochapwa limekwisha
(g) Barabara iliyofunguliwa imekamilika
(h) Magonjwa yaliyowasumbua yalitokana na athari ya mvua
(i) Ng'ombe aliyeangukia shimoni ameokolewa

6. Eleza kwa kifupi maana ya nahau zifuatazo:
(a) Juma ana mkono wa birika
(b) Kaka amepata jiko
(c) Mjomba amepiga maji
(d) Mwizi amekata mguu
(e) Mtoto amevimba kichwa
(f) Beka ana mkono mrefu
(g) Rafiki yangu anakaza kamba
(h) Kijana amepiga kete
(i) Huyu ana damu mbichi

7. Eleza kwa kifupi sifa sita zilizokifanya Kiunguja kusanifishwa na kuwa lugha sanifu ya Kiswahili.

8. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata.

Kwa hakika mwaka ule watu walivuna sana. Haikuwahi kutokea takribani kwa kipindi cha muongo mmoja hivi kuwa na mavuno kiasi hicho. Maghala yalijaa mahindi, mtama, mpunga, uwele, mbaazi, maharage, njegere na njugumawe. Nyama nyingi ililetwa kutoka porini ambapo wanawake walizitanda na kuzikausha motoni. Aidha, samaki wakubwawakubwa walipatikana kwa wingi, samaki ambao hawakuwahi kupatikana hapo awali. Kila mmoja kijijini hapo alikuwa na furaha.

Mavuno hayo yaliambatana na sherehe za mwisho wa mwaka ambazo zilikuwa ni zenye kufurahisha. Vigelegele vilisikika, ngoma zilipigwa na marimba yakavuma kijijini huku watu wa rika zote wakicheza bila kujali kuwa ni wazee au watoto. Wasichana wa umri wa miaka kuelekea kumi na mbili walitikisa miili yao kwa mvuto, huku miguu yao ikifuata mitindo maalumu kutoka ardhi ngumu yenye vumbi, wakicheza kwa madoido wakizungusha shingo zao kama twiga mbugani. Walipeana zamu ya kucheza wengine wawiliwawili na wengine watatuwatatu. Baadaye, wavulana nao walicheza ngoma yao. Kadiri ngoma zilivyodundwa, ndivyo vijana walivyokuwa wakicheza na kuruka juu kama swala. Wazee walitazama na kuridhika huku wanawake wakishangilia kwa vigelegele wakati vijana walioishiwa pumzi wakiondoka jukwaani.

Wakati wanawake na vijana wakicheza na kuimba, wazee waliketi kando ya moto wakinywa sharubati mpya. Mmoja baada ya mwingine, wazee hao walisimama na kuanza kucheza. Wakajisikia vijana kwa mara nyingine tena. Ingawa hawakuwa na kasi kama vijana, lakini waliwapiku katika mvuto na ubunifu wa uchezaji wao.

Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

Wapigaji watatu wa marimba walijitokeza na kuonesha umahiri wao. Kila mpigaji alionesha uhodari wake wa kupiga marimba, kuimba na kucheza. Alipoacha, mwingine alijitokeza, akiimba na kujiunga na tungo iliyoanzishwa. Walikuwa kama kundi la muziki wa wapiga marimba ambao kila aliyewasikiliza alivutiwa na upigaji wao uliotoa mlio wa kumtoa nyoka pangoni. Mdundo wa mziki wa marimba uliingia moja kwa moja hadi ndani ya mioyo yao.

Wakati wa machweo, watu walipumzika na kula chakula. Wapiga marimba waliungana na wapiga ngoma na hivyo uchezaji uliendelea tena hadi usiku wa manane. Kilichowaondoa watu uwanjani pale ni ama uchovu au usingizi.

**Maswali**

(a) Andika kichwa cha habari uliyoisoma kisichopungua maneno matatu na kisichozidi maneno matano.

(b) Bainisha shughuli mbili muhimu zilizokuwa zikiwapatia watu riziki kulingana na habari uliyosoma.

(c) Fafanua kwa kifupi maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika habari uliyoisoma.

  (i) Muongo mmoja

  (ii) Waliwapiku

(d) Fupisha habari hii kwa maneno yasiyopungua mia moja (100) na yasiyozidi mia na tano (105).

## SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka katika sehemu hii. Swali la **tisa (9)** ni la lazima na kila swali lina **alama 15**.

9. Jifanye wewe ni mmojawapo wa watoto waliohudhuria kongamano lililohusu haki za watoto. Andika beti tano za utenzi kuhusu "Haki za Mtoto."

**ORODHA YA VITABU**

**RIWAYA**

| | | |
|---|---|---|
| **Takadini** | - | Ben J. Hanson (MBS) |
| **Watoto wa Mama N'tilie** | - | E. Mbogo (H.P) |
| **Joka la Mdimu** | - | A. J. Safari (H.P) |

**TAMTHILIYA**

| | | |
|---|---|---|
| **Orodha** | - | Steve Reynolds (MA) |
| **Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe** | - | E. Semzaba (ESC) |
| **Kilio Chetu** | - | Medical Aid Foundation (TPH) |


Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

10. Lengo kuu la kazi za fasihi ni kuonya na kuiasa jamii. Thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja tatu kwa kila riwaya kutoka katika riwaya mbili ulizosoma.

11. "Uzembe ni jambo linalokwamisha maendeleo ya jamii nchini Tanzania." Tathmini kauli hii kwa kutoa hoja tatu kwa kila tamthiliya kutoka katika tamthiliya mbili ulizosoma.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org